Radio Scripts: Women Talk Peace in Swahili

Wanawake wa kiAfrica na azimio 1325 kuhusu wanawake,amani na usalama.
Makala ya redio kuhusu azimio 1325 la Baraza la Usalama wa Umoja wa Mataifa—lliyohusisha mazungumzo ya amani ya mwaka 2005, yaliyoendesha kwa njia ya mtandao.

10.48 madakika

SFX: Blasts, gunshots, children crying

1. Sadia: Mama! Mama! Mamaaa! Nisaidie! Jamani nisaidieni! Mtu yeyote anisaidie! Oh! Mungu wangu! Tafadhali muokoe bwanangu. Nimebakiza yeye tu. Oh mungu wangu! Tafadhali.

2. Juma: Salim!, Salim, amka, Njoo ndugu yangu. Najua waweza kuvuka talizo hili. Una nguvu… ni jeraha tu la risasi. Salim! Usifie mbele yangu. Usifanye hivyo Usifie mikononi mwangu. Itakuwaje kwa mkeo na watoto? Nimetenda nini ili kuangukiwa haya? Basi, mniue tu ninyi wanamgambo wakatili mkiwa na bunduki, mwataka kuuatu kila mtu, hata wasio na hatia.

3. Juma: Tafadhali Sadia, kwa ajili ya watoto, kimbia utoke hapa, uokoe maisha yako. Ondoka haraka! Salim hayuko tena. Wamemwua (wamemuua)

4. Sadia: Nawachukia! Siwataki! Siwapendi (huku akilia – sauti yake ikikatwakatwa na mziki wa kiutamaduni).

5. Msimlizi (wa kike): Huzuni kubwa zinazomkabili Sadia kuhusu kifo cha bwanake baada ya majambazi wa bunduki kuvamia kijiji chao. Sadia na wanawe saba wameona majambazi wakikata mmio wa bwanake katika uvamizi wa usiku. Wao ni waathiriwa wa hivi karibuni katika mkoa wa Darfur kwenye nchi tajiri ya mafuta ya Sudan. (Hata wilayani Gulu, kaskazini mwa Uganda) (Ingiza mziki wa kiutamaduni, kisha sauti ififie pole pole na inyanyaliwe tena).

6. Msimlizi (wa kiume): Hadithi na visa vya ukweli na maumivu kama hicho cha Sadia, hutokea kila siku. Vita vya ajabu na ukweli hususan katika eneo la Sahara nusu jangwa la Afrika, hasa hasa katika pembe la Afrika na maeneo ya maziwa makuu. Katika hali hii ya vituko, wamawake na watoto hubaki wakihangaika na maswali mengi pamoja na matatizo.

7. Msimlizi (wa kike): Sierra Leone, Liberia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Rwanda, Angola, Sudan, Ethiopia, Eriterea, Somalia na kaskazini mwa Uganda, ni baadhi ya nchi zinazoshuhudia vita, ambapo wanawake wamekuwa katika huzuni na mateso mengi yanayosababishwa na bunduki, kwa hivyo si jambo baya kusema kwamba huu ni wakati unaofao kwa mwanamke wa Afrika kusimama imara, apigane dhidi ya vita, siyo kwa kutumia bunduki na panga au jambia, bali kwa kutafuta nafasi kwenye meza ya kujadilia amani.

8. Msimlizi (wa kiume): Mara nyingi wanawake hutamka juu ya uhasama katiika maisha yao kuhusu vita, na jinsi vita vinavyoeneza uhasama katika jamii zao, na jinsi uhasama unvyoshuhudiwa kwa njia mbali mbali na wanawake na wanaume. Jamii nyingi huwa na fikra za kijeshi katika vita vya wenyewe kwa wenyewe na hali hii ya kuishi kijeshi huwakalia watu kwa mda mrefu. Wanajeshi hupanda mbegu ya uhasama katika vita virefu, na mbegu hii, ni vigumu kuifuta.
Hali hii ya uhasama huyafanya maisha yawe magumu mno na ya hatari kwa wanawake, hususan kwa usambazaji wa silaha ndogo za bei nafuu.

9. Msimlizi (wa kiume): uhasama dhidi ya wanawake haukomi tu baada ya kuweka sahihi kwenye mapatano ya kukomesha vita, kwa ukweli, uhasama huendelea na kuzagaa. Twaweza kufanya je ili kujilinda nyakati za misuko-suko, na baadaye? Twawezaje kuzuwia uhasama? Twawezaje kuwasaidia wanawake wapone mateso ya ubongoni na mwilini? Nchini Kenya, ambapo kuna utulivu angalao, ukilinganisha na majirani wake, visa vya kuwabaka wanawake na wasichana, vinazidi kushududiwa katika sehema zote za jamii.

10. Msimlizi (Wa kiume): Hadi hivi karibuni mmoja kati ya matokeo yasiyo wazi ya mizozo ya kivita, ni uhasama dhidi ya wanawake. Katika nchi ambazo zimechafuliwa na mazingira ya kivita uchumi na mazingira vyote vimeharibika, kwa hivyo umalaya ndiyo inakuwa kazi kwa wanawake ili waweze kuishi. Hata katika kembi maalum za wakimbizi ambako watu wananusurika kutoka kwa vita, umalaya wa kulazimishwa hutokea mno, kuwabuka wanawake kunakuwa kama chombo cha vita. Je, hali ni lazima iwe hivyo?

11. Msimlizi (wakike female): Hapana! Si lazima hali iwe hivyo. Kilichokuwa kama siri bila kubainika pia, sasa kinajadiliwa kwenye ngazi za juu sana. Mwezi oktoba mwaka wa 2000 Baraza la Usalama la Umoja wa mataifa lilipitisha ibara ya kimapinduzi katika azimio la 1325. Hili ni azimio la kwanza lililowahi kupitishwa na Baraza la Umoja wa mataifa linalohusu

hasa madhara ya kivita kwa wanawake, na michango ya wanawake kwa kutatua mizozo na amani ya kutegemewa/kwuendelezwa.

Azimio hilo latilia mkazo dhima ya wanawake katika kuzuwia mizozo ya kivita/silaha, umuhimu wa usawa. Katika kushiriki kwenye juhudi zote za kutunza amani na usalame, na ile haja ya kuwalinda wanawake mnamo nyakati za mizozo ya kivita. Mada hizi tatu katika azimio 1325 yaani: kushiriki uzuwiaji (Kuzuwia) na kulinda, nazo zahitaji mataifa yanachama katika umoja wa mataifa, kuona kwamba wamawake wanawakilishwa katika shuguli zote za kuchukua uamuzi kuhusu maswala ya amani na usalama.

Hapa tupo naye Jesica Nkuuhe Naibu Mkrugenzi wa shirika la Isis WICCE ambaye anaweza kufafanua jinsi wanavyotumia azimio la 1325 ili kuhakisha kwamba wanawake wa Uganda wanashiriki katika majadiliano yote ya amani na usalama.

12. Jessica Nkuuhe (JN): Tangu Isis WICCE waanze kushirikiana na watumiao azimio la 1325 baada tu ya kupitisha azimio hilo mwezi oktoba 2000, Isis WICCE ilizingatia hasa kuwawezesha wanawake kufahamu azimio hilo. Kwa hiyo, ikiwa schemu ya mafunzo yetu, tunashirikisha maswala ya sheria za kimataifa za kiutu, na kuwapa wanawake mbinu bora za kutumia katika kushauriana na kujadiliana; mbina za kufahamu, kuchambua na kutanzua mizozo, pamoja na mbinu za utetezi, Lengo kuu ni kuona kwamba wakialikwa kwenye meza za majadiliano, watakuwa mbinu zinazohitajika katika zoezi hilo /shuguli hiyo.

Wakati huo huo, shirika hili limekuwa likikusanya taarifa juu ya uzoefu wa wanawake katika hali za kivita, ili tuweze kuonyesha aina za mizozo hiyo na ukubwa wenyewe wa mizozo. Aidha tukiwa na wanawake wengine, tunaweza kujiunga kwa kampeini ili kuelowa aina hiyo ya uhasama dhidi ya wanawake katika hali za kivita.

Tumeweza kuzalisha/kutoa taarifa za magazetini na zile za video kuhusu uvunjaji haki za wanawake husasan zile za kujamiana, na mateso ya kimawazo yanayowafikia wanawake katika hali za kivita.
Pia wanawake wa Uganda tunawapa uwezo wa kushiriki katika mijadala ya kimataifa kwa mfano ile ya kujenga amani ile ya “cyber” (ya kimatandao) kama ule mkutano alioandaliwa kama Jopo La Wanawake (IWTC) katika kikao cha Baraza la umoja wa mataifa cha Oktoba 2005.

13: Msimlizi (wa kiume male): Hapo awali ilitajwa kwamba azimio la 1325 pia linayataka mataifa yanachama kuhakikisha kuwa wanawake ni lazima washiriki katika shuguli zote za kuchukua uamuzi juu ya amani na usalama. Sasa hivi tuna Rais wa kike wa kwanza katika bara la Afrika nchini Liberia, Hii ina umuhimu gani Jessica?
14. JN: Jambo hili ni muhimu kwa sababu uchaguzi wa Bi Ellen Johnson nchini Liberia,umethibitisha wanawake wanaweza kufikia malengo yao wakijiandaa vizuri. Hali hii inaonyesha pia kwamba wanawake na wanauwe wana imani na viongozi wanawake.

Katika hutuba yake ya mwanzoni baada ya kuchaguliwa, Bi Johnson alibainisha kwamba, kuchaguliwa kwake kulitokana na nguvu ya wanawake hasa wafanyabiashara wadogo katika masoko na wanawake wengine wa kiwango cha chini cha maisha. Kwa hiyo alithibitisha kwamba mchango wa wanawake wa kipato cha chini ni muhimu sana katika maendeleo.

Jambo hilo ni la busara mno kwa sababu, inanibidi niongeze kwamba michango ya wanawake wa daraja za chini, nayo ni ya busara mno. Katika mwaka wa 2004, shirika la Isis WICCE lilitoa video yenye taarifa kuhusu juhudi za ajabu za wanawake katika Afrika ili kuonyesha hasa nini wanawake wanachofanya katika uwanja wa kujenga amani kuanzia daraja za chini…
Tukiwa na wabuni-sera wa kiwango cha kitaifa, ni lazima tuonyeshe kwamba kuna wanawake wenye uwezo wa kuongoza, ubainifu huo ufikie hata ule umoja wa Afrika (AU), na hata kwenye kiwango cha kimataifa, hususan katika uwanja wa kutatua mizozo, ule wa kujenga amani. Wa kwa hivyo wanawake hao, wanaweza kushiriki vizuri kuliko hata wanaume katika mijadala ya amani, kwa hivyo, ile kadhia ya kusema kwamba hakuna wanawake wenye uwezo wa kutenda jambo, haina maana kamwe.

Ni jambo la busara mno kuwashirikisha wanawake wanaostahili na kuwafunza wanawake wanaostahili na kuwapata wanawake wanaofaa kuwekwa katika nyadhifa za uongozi, kwa sababu, siyo kila mwanamke aliye na dhamira ya kuhakikisha kuwa haki za wanawake zalindwa na kupandishwa na kuheshimiwa. Sisi katika Afrika, tuna wajibu mkubwa kuhakikisha kuwa yaliyomo kwenye azimio la 1325 la umoja wa mutaifa yanatekelezwa.

Ni lazima tuwafikie wanawake wengi kadri tuwezavyo, hususan wanaoishi katika sehemu za misukosuko, ili waweze kutumia azimio hili kudai haki zao, na ile furusa ya kujenga amani katika jami. Hii, ni sheria, inaanza sasa. Imeanza nasi.

15. Msimlizi (wa kike): Pata taarifa,Saidia wanawake kushiriki katika kuzuia,kutatua migogoro na kujenga amani.Tuwashirikishe dada zetu wa kiafrika katika meza ya amani. Saidia ushiriki wa wanawake katika kutatua migogoro

na kujenga amani.Tembelea kituo hiki ili kujifunza zaidi kuhusu baraza la usalama la umoja wa mataifa na azimio la 1325 na kwa vipi linaweza kutumika katika jamii yako.

Ujumbe kutoka katika kituo Cha Jopo la Wanawake la Kimataifa (IWTC) likishirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari wanawake nchini Uganda(UMWA) chini ya ufadhili wa Idara ya mashauri ya kigeni na shirika la mpango wa Usalama wa Kiutu nchini Canada (Human Security Program in the Department of Foreign Affairs and International Trade, Canada) na shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Wanawake (United Nations Development Fund for Women) na Wizara ya Mashauri ya Kigeni ya Uholanzi (Netherlands Ministry of Foreign Affairs) na kituo hiki.

Music unaingizwa na unafifia

Yameandikwa na Lillian Odera
Yakasahihishwa na Mavic Cabrera-Balleza

Charity na Nora,marafiki wawili wanaojihusisha na harakati za kuleta amani
Makala ya redio juu ya mikakati ya kitaifa kuhusu azimio 1325 la Baraza la Usalama wa Umoja wa Mataifa
6. 23 madakika

Gonga mlango/bisha hodi

1. Charity: Hodi!Hodi!Kuna mtu yeyote nyumba hii?

2. Nora: Oh!Charity ingia,ingia ukae,Ndio kwanza tu nimewasha birika.

3. Charity: Asante Nora,mlio wake washangaza,nilikuwa na wakati mgumu.

4. Nora:Nimefurahi kukuona, ni muda mrefu hatujaonana, lakini mwishoni hivi vita vitakoma na miongoni mwetu sisi tuliobaki tuanze kuweka maisha yetu pamoja.

5. Charity: Ndio, ulikuwa wakati mbaya.Vita na ukatili havitatufikisha popote.Familia yako haijambo?

6. Nora: Ndio nashukuru Mungu wote wazima wa afya,na Familia yako je?

7. Charity: Ndio Familia yangu haijambo pia.Unajua Nora,hiyo ni moja ya sababu zilizonileta leo hii,pamoja na kukuona nilikuwa nafikiria kuwa sisi ni miongoni mwa wenye bahati,tunatakiwa kutafuta njia ya kusafisha barabara ili kutafuta amani ya nchi yetu.Nilitaka kukuambia mawazo mapya niliyonayo.

8. Nora: Kweli, mara nyingi mawazo yako huwa mazuri Charity,nini kimetokea?

9. Charity: Sawa,umeshasikia kuhusu azimio jipya la1325 la umoja wa mataifa?

10. Nora: Ndio,nimeshasikia toka katika moja ya mikutano ya shirika letu.Inahusu ushirikishwaji wa wanawake katika kujenga amani,ni kweli?Lakini niwe muwazi sijui ni jinsi gain tutatumia sera hiyo katika nchi yetu.

11. Charity: Sawa,nafikiri maendeleo yatakuwa mazuri kwa sababu kuna mazungumzo juu ya azimio la 1325 yanayolenga katika kuendeleza mipango ya kitaifa kupitia uzoefu wetu wanawake na kwa vipi tunashiriki na sio tu katika kujenga amani bali pia katika kuzuia migogoro.Mpango wa kitaifa wa azimio la 1325 pia utasaidia serikali kujiwekea majuku ya uswa wa kijinsia katika kutatua migogoro.Hii inamaanisha kutoa fedha na rasili mali nyingine katika kusaidia juhudi za wanawake za kutafuta amani kuanzia ngazi ya chini ya jamii.

Niamini Nora nadhani tuna chombo cha kutusaidia kufanya mabadiliko.Hili ni jambo la kushtua.tunatakiwa kutimiza vitu vitatu ambavyo ni kuwalinda wanawake katika migogoro,kuzuia ukatili dhidi yao na kuhakikisha wanashiriki katika kufanya maamuzi na kulinda amani kupitia mpango wa maendeleo ya taifa.

Kuna nchi nyingi barani Afrika mbili miongoni mwa hizo zina hali mbaya lakini ya tatu nadhani tunaweza kuibadilisha.Nimekuwa nikiwaza sana kuhusu jambo hili na nimeshaanza kuongea na baadhi ya watu.

Tunakiwa kushiriki katika kuendeleza mpango wa taifa ili tuwezw kulinda amani na hata kuzuia migogoro ya hapo baadae kama tutakuwa na sauti.

12. Nora: Umepatia Charity.Wanahitaji sauti na mchango wetu.Angalia wanawake wanavyohainga nah ii migogoro.Tuna mahitaji tofauti na wanaume, tunajaribu sana kuwalinda watoto wetu.Wengi wetu walikuwa wakibakwa na wengine kufa.Mwanzo wanawake wangetakiwa kuzuia migogro na kujenga amani katika hiki kipindi cha hatari.

Kuna maana kubwa sana kufanya kazi na huu mpango wa taifa.Tungeisaidia serikali ili ielewe suala la usawa wa kijinsia na migogoro kabla, sasa na hata baadae,au unaonaje hiyo?

13. Charity: Kwanza kabisa inaweza kuleta pamoja wizara na idara za serikali ambazo zilikuwa hazingumzii suala hili achilia mbali suala la jinsia.Waweza kuwakuta wakiongea na mashirika mengine ambayo yatakuwa yakivutiwa na mambo haya.Twaweza pia kupata makundi ya wanawake pamoja yakishirikiana na wanasheria wanawake na vikundi vya haki za binadamu kuhakikisha tunapata nafasi ya kufanya maamuzi bila kusahau wanawake ambao tayari wapo serikalini na tunahitaji wanaume ambao wana uchungu na suala hili.

14. Nora: Unajua kitu kinachofurahisha ni kuhusu mpango wa taifa ambao kwa kweli ni chombo kikubwa kinachoweza kusaidida serikali yetu.

15. Charity: Ndio Serikali imeanza kugundua kuwa vikundi vya wananchi vina umuhimu nimesikia kuna baadhi ya nchi barani Afrika zimeanza moja kwa moja kutumia vikundi vya wananchi kwa ajili ya kupata mafanikio.Unajua kuna mambo mengi,serikali inafanya mipango ya kubadilisha ili kupata uzoefu wa usawa wa kijinsia na nina uhakika hawana wasiwasi na hilo.

16. Nora:Kwa hiyo unafikiri ni kitu gani cha kufanya? Hatua yetu ya kwanza ni ipi? Hebu tupange.

17. Charity: Kwanza tuwaite baadhi ya wanawake na makundi mengine,tuongee na watu wachache mmoja mmoja wote wake kwa waume halafu tuone kama tutapata mkutano.....

18. Msimulizi: Wanawake na wanaume kama Charity na Nora wapo wengi kuzunguka Afrika.Hatimaye wanacho chombo cha kutumia katika kuwasaidia wanawake wasio na sauti na wenye nguvu katika maamuzi kuhusu kulinda na kujenga amani.Wewe na kundi lako,na mahali unapoishi mwaweza kuwa na sauti.Wanawake wanaumizwa na migogoro ya aina nyingi tofauti kabisa na wanaume.Wanawake wana nafasi kubwa kutumia uzoefu na ukarimu kusaidia katika kuzuia migogoro,kujilinda wao wenyewe na wasichana katika hali zote za migogoro na pia wanawake wana umuhimu mkubwa katika kubadilisha na kuilinda amani.

19. Msimulizi: Pata taarifa,Saidia wanawake kushiriki katika kuzuia,kutatua migogoro na kujenga amani.Tuwashirikishe dada zetu wa kiafrika katika meza ya amani. Saidia ushiriki wa wanawake katika kutatua migogoro na kujenga amani.Tembelea kituo hiki ili kujifunza zaidi kuhusu baraza la usalama la umoja wa mataifa na azimio la 1325 na kwa vipi linaweza kutumika katika jamii yako.
Ujumbe kutoka katika kituo Cha Jopo la Wanawake la Kimataifa (IWTC) likishirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari wanawake nchini Uganda(UMWA) chini ya ufadhili wa Idara ya mashauri ya kigeni na shirika la mpango wa Usalama wa Kiutu nchini Canada (Human Security Program in the Department of Foreign Affairs and International Trade, Canada) na shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Wanawake (United Nations Development Fund for Women) na Wizara ya Mashauri ya Kigeni ya Uholanzi (Netherlands Ministry of Foreign Affairs) na kituo hiki.

Yameandikwa na Maggie Range
Yakasahihishwa na Mavic Cabrera-Balleza

Ulijua kwamba?
Utangulizi kuhusu azimio 1325 la Baraza la Usalama wa Umoja wa Mataifa

1.38 madakika

Ulijua kwamba miaka mitano iliyopita Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lilipitisha azimio juu ya manawake katika maswala ya amani na usalama?Azimio hilo,azimio la 1325,linawataka wanawake kushiriki kuzuia migogoro,kutatua migogoro na kujenga amani.

Azimio hili limekuja kwa wakati .Wanao athirika vibaya na migogoro ya kutumia silaha ni wanawake na watoto,mfano mwaka 2003-2005 jumla ya watoto 13000 walitekwa katika wilaya za Gulu,Kitgum na Pader kaskazini mwa Uganda kufuatia vita kati ya waasi wa Lord's Resistance Army (LRA) na majeshi ya serikali.

Kutokana na historia hii ni lazima wanawake wawe sehemu ya kutatua migogoro.
Azimio 1325 linawataka wanawake kushiriki katika kupanga maamuzi na majadiliano ya amani.

Hii ni rahisi kusema kuliko kutenda. Sisi wanawake tumekuwa tukijifunza kwa masuala ya amani na usalama ni shughuli ya wanaume peke yao. Wanaume hawajui kama wanawake pia wanahusika kwenye mazungumuzo ya amani, na sisi wanawake tunaridhika kutokuwepo.Hali hii inatakiwa kubadilika.

Saidia wanawake kushiriki katika kuzuia na kutatua migogoro pamoja na kujenga amani.

Ujumbe kutoka katika kituo Cha Jopo la Wanawake la Kimataifa (IWTC) likishirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari wanawake nchini Uganda(UMWA) chini ya ufadhili wa Idara ya mashauri ya kigeni na shirika la mpango wa Usalama wa Kiutu nchini Canada (Human Security Program in the Department of Foreign Affairs and International Trade, Canada) na shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Wanawake (United Nations Development Fund for Women) na Wizara ya Mashauri ya Kigeni ya Uholanzi (Netherlands Ministry of Foreign Affairs) na kituo hiki.

Yameandikwa na Mavic Cabrera-Balleza